

Kwanini kuwe na kitabu Cha kumbukumbu la Torati na kwanini
kiitwe vile?

Kitabu hiki katika lugha ya kiebrania kinasomeka kama “Devarim”
ambayo tafsiri yake ni “Maneno”

Na ndio maana mstari wa kwanza kabisa un itaanza Kwa kusema. “Haya
ndiyo maneno”

Kumbukumbu la Torati 1:1

*[1]Haya ndiyo maneno Musa aliyowaambia Israeli wote ng'ambo ya
Yordani barani, katika Araba lilioelekea Sufu, kati ya Parani, na
Tofeli, na Labani, na Hazerothi, na Dizahabu.*

Lakini katika tafsiri ya kigiriki Cha kale (septuagint), kilisomeka kama
“deuteronomioni” chenye maana ya “Mrudio wa sheria” ambapo Kwa
sisi kinasomeka kama “kumbukumbu la sheria/torati”.

Ni kitabu Cha Tano ambacho kiliandikwa na Musa karibia na mwisho wa
Ile miaka 40, wakati walipokuwa ng'ambo ya Yordani katika nchi ya
Moabu.

Lengo la kuandikwa kitabu hicho ni kukumbushwa sheria na maagizo ya

Kwanini kuwe na kitabu Cha kumbukumbu la Torati na kwanini
kiitwe vile?

Mungu, kwasababu kundi kubwa la Wana wa Israeli lililopokea sheria
Kule mlima Sinai mwanzoni, lilifia jangwani, hivyo kile kizazi kipy
Hakikuwa na msingi imara juu ya sheria za Mungu. Na ndio hapa Musa
anaagizwa na Mungu awakumbushe Wana wa Israeli sheria yake.

Kitabu hiki kimeanza kuwakumbushia safari Yao Toka Misri, pia
kikagusia jukumu lao la kumpenda Mungu na kuzishika sheria zake.
Ikafuatana na baraka na laana ambazo zitampata mtu katika kutii au
kutokutii, na mwisho kifo cha Musa.

Je ni Nini tunajifunza kuwepo kwa kitabu hiki ?

Bwana anataka na sisi tuweke kumbukumbu la agano lake moyoni
mwetu, Kwa vizazi vijavyo tupende kuwafundisha vizazi vinavyochipukia
Neno la Mungu, tusiwaache tukadhani wataelewa tu wenyewe kisa
biblia ipo, bila kukumbushwa Kwa kufundishwa.

Musa alifanya vile ndio maana kizazi kile kikawa imara baada ya pale.

Na sisi tuwe watu wenye tabia hii, Sio kwa watoto tu hata Kwa kondoo
wa Bwana kanisani. Mara Kwa mara tuwakumbushe maagizo ya Mungu.

Kwanini kuwe na kitabu Cha kumbukumbu la Torati na kwanini
kiitwe vile?

Kwa maelezo ya ziada kuhusu kitabu hichi pitia hapa >>>

<https://wingulamashahidi.org/2019/05/13/vitabu-vya-biblia-sehem-u-ya-2/>

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:

Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au

Piga namba hizi: +255789001312 au +255693036618. **Jiunge na magroup yetu ya whatsapp kwa kubofya hapa > WHATSAPP-Group**

Mada Nyinginez:

Vitabu vya Deuterokanoni ni vya ki-Mungu?

VITABU VYA BIBLIA: Sehemu ya 1

Mtiririko wa vitabu vya biblia kwanini upo vile?

Je! Mwendo wa Sabato ulikuwaje kibiblia?(Matendo 1:12)

Kwanini kuwe na kitabu Cha kumbukumbu la Torati na kwanini
kiitwe vile?

NJIA YA WOKOVU NDANI YA KITABU CHA WARUMI.

Nini maana ya “Atamwangamiza kwa ufunuo wa kuwapo kwake”.
(2Wathesalonike 2:8).

Rudi nyumbani

Share on:

WhatsApp